

Family ID Number: \_\_\_\_\_ Participant Name(s): \_\_\_\_\_

## WIC Haki na Majukumu

Tunataka kuhakikisha kwamba unaelewa haki na majukumu ya mshiriki wa WIC. Haki na majukumu ya WIC pia hutumika ikiwa unapokea faida za Farmers' Market Nutrition Program (Mpango wa Lishe ya Soko wa Wakulima, FMNP) ya WIC. Haki na majukumu ya FMNP ni pamoja na, lakini si tu, heshima na kutendewa kwa adabu kutoka kwa wauzaji wa FMNP na kutumia faida za soko za wakulima kama inavyoelekezwa na wafanyakazi wa WIC.

### Haki Zangu

- **Vyakula vya WIC:** Ikiwa ninahitimu kwenye WIC, nitapata kadi ya eWIC ya kununua vyakula vyenye afya. WIC hutoa baadhi, lakini sio yote, chakula/fomula kila mshiriki anahitaji.
- **Maelezo ya lishe:** Nitapata habari kuhusu kula lishe ya afya na kutokuwa mzembe.
- **Msaada wa kunyonyesha:** WIC itanisaidia na kunitia moyo kwa kunyonyesha.
- **Maelezo ya huduma ya afya:** Nitapata habari kuhusu chanjo, kupata huduma za afya, na huduma zingine ambazo niko na hamu nazo.
- **Kutendewa kwa haki:** Sheria za kuandikishwa kwenye WIC ni sawa kwa kila mtu. Ninaweza kuomba haki ya kusikilizwa kama mtu ameniambia siwezi kuandikishwa kwenye WIC na sikubaliani nayo.
- **Ungwana wa kawaida:** WIC na wafanyakazi wake watanitendea kwa ungwana na heshima. Ninaweza kuwaambia wafanyakazi wa WIC ikiwa sijatendewa kwa heshima.
- **Maelezo ya uhamishaji:** Ninaweza kuhamisha WIC yangu kwenda kliniki au jimbo jingine. Naweza kuomba karatasi ya uhamisho.
- **Mpango wa Lishe ya WIC hauna ubaguzi:**

Kwa mujibu wa sheria ya shirikisho ya haki za kiraia na sheria na sera za haki za kiraia za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), taasisi hii hairuhusiwi kubagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia (ikiwa ni pamoja na utambulisho wa kijinsia na mwelekeo wa kijinsia), ulemavu, umri, au kulipiza kisasi kwa kuhusika katika shughuli za awali za haki za kiraia.

Maelezo ya mpango yanaweza kupatikana katika lugha zingine isipokuwa Kiingereza. Watu wenye ulemavu wanaohitaji njia mbadala za mawasiliano ili kupata maelezo ya mpango (km, Breli, maandishi makubwa, kanda ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani), wanapaswa kuwasiliana na Shirika husika la Jimbo au la eneo linalotoa mpango au Kituo cha TARGET cha USDA katika (202) 720-2600 (sauti na TTY) au wawasiliane na USDA kupitia Huduma ya Uelekezi ya Shirikisho (Federal Relay Service) katika (800) 877-8339.

Ili kuwasilisha malalamiko ya ubaguzi katika mpango, Mlalamishi anapaswa kujaza Fomu ya AD-3027, Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi wa Mpango wa USDA ambayo inaweza kupatikana mtandaoni katika: <https://www.fns.usda.gov/sites/default/files/resource-files/ad3027-swahili.pdf>, au kutoka ofisi yoyote ya USDA, kwa kupiga simu (866)-632-9992, au kwa kutuma barua kwa USDA. Barua lazima ijumuishishe jina, anwani, nambari ya simu ya mlalamishi, na maelezo ya maandishi ya madai ya kitendo cha ubaguzi kwa undani wa kutosha ili kumfahamisha Katibu Msaadizi wa Haki za Kiraia (ASCR) kuhusu asili na tarehe ya madai ya ukiukaji wa haki za kiraia. Fomu au barua iliyojazwa ya AD-3027 lazima iwasilishwe kwa USDA kupitia:

- (1) **barua:**  
U.S. Department of Agriculture  
Office of the Assistant Secretary for Civil Rights  
1400 Independence Avenue, SW  
Washington, D.C. 20250-9410; au
- (2) **faksi:**  
(833) 256-1665 au (202) 690-7442; au
- (3) **barua pepe:**  
[program.intake@usda.gov](mailto:program.intake@usda.gov)

Taasisi hii ni mtoa huduma asiyebagua.

## Habari Zilizoshirikishwa

### Habari zako zinaweza kushirikishwa:

- Na programu nyingine za WIC ukihama.
- **Na programu nyingine za umma ambazo zinaweza kukusaidia. Unaweza kuuliza kuona orodha ya programu hizi.**
- Kama ilivyohitajika kisheria

## Majukumu yangu

### Ninakubali kutoa maelezo ya kweli na kamili kuhusu:

- Utambulisho wangu, hali ya ujauzito, hali ya kunyonyesha, anwani, na nambari ya simu.
- Mapato yangu ya kaya.
- Idadi ya watu wanaoishi katika nyumba yangu.
- Kuwa kwenye Medicaid, FoodShare (mihuri ya chakula), TANF (Temporary Assistance to Needy Families), au FDIPIR (Food Distribution Program on Indian Reservations).

### Ninakubali kufuata sheria zilizopo hapa chini. Nita:

- Pata msaada kutoka kwa kliniki moja tu ya WIC kila mwezi.
- Ripoti kadi yangu ya eWIC au pampu ya maziwa ya WIC iliyopotea au liyoibiwa kwa wafanyakazi wa WIC.
- Hakikisha mtu yeyote ninayemtaja kutumia kadi yangu ya eWIC anajua sheria za WIC. Nitamfundisha jinsi ya kutumia kadi yangu ya eWIC kwa usahihi.
- Weka miadi yangu ya WIC au kupiga simu kwa kliniki ili kuratibu upya.
- Tumia vyakula na fomula ya WIC tu kwa mtu kwenye WIC na kuhakikisha vyakula vinaenda na mtu kwenye WIC wakati wa malezi wa pamoja, malezi ya utunzaji, nk.
- **Kutouza, kupeana, au kutoa kadi yangu ya eWIC, vyakula au fomula, au pampu ya matiti ya WIC.** Ikiwa nina vitu vya WIC ambavyo siwezi kutumia, nitazirejesha kwenye kliniki.
- Kutofanya biashara na/ kubadilishana au kurudisha kadi yangu ya eWIC, vyakula au fomula, au pampu ya matiti za WIC kwa fedha, mikopo, ahadi, au vitu vingine.
- **Kutochapisha vitu vya WIC kwenye mtandao.**
- Fuata kanuni katika Mwongozo wa Ununuzi wa WIC.
- Kutoapa, kupiga kelele, kunyanyasa, kutishia, au kudhuru kimwili wafanyakazi au duka ya WIC.
- Kutojifanyia malipo yangu binafsi, isipokuwa katika foleni ya malipo za kibinafsi, ikiwa nimeajiriwa na duka ya WIC.

### Makubaliano: Ninapaswa kukubaliana na vitu hivi kuwa kwenye WIC:

- Maelezo yote niliyopatia WIC ni ya kweli. Nitawaambia wafanyakazi wa WIC mara moja ikiwa kuna mabadiliko yoyote.
- WIC inaweza kuthibitisha ukubwa wa kaya yangu na vyanzo vyote vya mapato yangu ya kaya.
- Nikivunja sheria za WIC mimi au mtoto wangu, tunaweza kuondolewa kwenye WIC.
- Nikisema uongo au kuficha ukweli ili kupata vyakula vya WIC au nikose kurudisha pampu ya matiti niliyokopeshwa, nitahitaji kulipa WIC thamani ya fedha za vitu hivi.
- WIC ni mpango wa msaada wa shirikisho. Nikivunja kanuni za WIC ninaweza kushtakiwa chini ya sheria ya kiraia au ya jinai kwa sheria ya serikali na shirikisho.

**Nimesoma fomu hii, au wafanyakazi wa WIC wamenisomea fomu hii. Ninaelewa na kukubaliana na kanuni na makubaliano yaliyo hapo juu, na nimepokea nakala ya haki na majukumu haya katika Mwongozo wa Ununuzi wa WIC.**

SAINI – Mshiriki/Mzazi/Mlezi/Mtoa huduma

Tarehe ya Saini